MTIHANI WA MWIGO WA ALLIANCE HIGH SCHOOL
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Bw. Kitau

1. UFAHAMU - MAJIBU
   (a) Ikolojia (1X1=1)
   (b) Elimu ya kisayansi inayohusu uhusiano wa kimazingira kati ya vitu vyenye uhai na visivyokuwa na uhai. (1X2=2)
   (c) Hujirekebisha kulingana na mazingira wanamoishi. (1X2=2)
   (d) - Ukanda wa istiwai una joto,mvua na unyevunyevu
       - Hufanya misitu minene yenye miti mirefu.
       - Kuna mimea ya kayanga inayotambaa na kukwea miti mingine.Ukanda wa savanna una joto na mvua kiasi. Sehemu nyingi ni vichaka na nyasi zisizohitaji mvua. (3X1=3)
   (e) Upepo una faida – husukuma mawingu yanayoleta mvua.
       Hasara - Upepo ukizidi hudhuru mimea na wanyama. (2X1=2)
   (f) (i) Matamvua – Viungo vya kupumua.
       (ii) Kusharabu hewa – Kuvuta hewa
       (iii) Istiwai – Ukanda ulio katika sehemu ya kati ya dunia. (3 X1=3)

2. MWONGOZO WA UFUPISHO
   a) - Hawakujua maisha yaliyowasubiri - raha / matatizo
      - Mazingira mapya yaliwapa wasiwasi
      - Uoga
      - Taharuki ya kumsubiri mkuu wa chuo
      - Mawazo mengi yaliwapita akilini
      - Kila kitu kilikuwa tofauti

      Zingatia hoja tano - alama 5
      Adhibu kila kosa la kisarufi na hijai

   b) - Mwalimu mkuu kuitwa Vice Chancellor
      - Nyumba ya kulala- Halls
      - Shule - Ndaki/ University
      - Waliposimama walishauriwa wakae

      **Zingatia hoja 2x1.**
      **Makosa ya kisarufi na hijai yaadhibiwe**

   c) - Mkuu wa chuo alipoingia walisimama kwa mjiko
      - Wakaashiriwa wakae
      - Wakacheka kwa adabu na heshima
      - Wakajisikia wamepoa
      - Kujuana kwa wageni na wenyeji
      - Ikawa siku njema kwao iliyoonekana mapema

      Zingatia hoja zozote 5x1 =5
      Makosa ya kisarufi na hijai yaadhibiwe

## MWONGOZO WA UFUPISHO

Maudhui
a) 5x1 = al 5
b) 2x1 = al 2
c) 5x1= al 5

Utiririko (Mtiririko) U = al 3
JUMLA ............... = al 15

Maudhui = hoja zinazohusu swali
Mtiririko = KADIRIA ALAMA za mtiririko kutegemea;

- jinsi hoja hizo zilivyowasilishwa/kueleweka kwa urahisi
- Idadi ya hoja alizopata
- Idadi ya makosa ya sarufi na hijai
- Usafi wa kazi
- Ukamilifu wa sentensi (asitumie vidokezo) wala ku orodhesha.
- Kutoorodhesha hoja

Mtiririko katika ufupisho si sawa na ule wa insha ambao huzingatia matumizi ya viunganishi bali ni ule ukamilifu wa hoja kisentensi hata kama ni sentensi fupi fupi.

- Akitumia vidokezo au kuorodhesha hoja kwa njia zozote kama kutumia nambari au vistari apate sufuri (0) katika mtiririko.

*Tuza Mtiririko baada ya swali zima si katika visehemu tofauti

*Mtiririko waweza kuwa juu ya wastani, wastani au chini ya wastani. Katika swali hili, tuza alama 1 ½ kwa juu ya wastani, 1 kwa wastani na ½ kwa chini ya wastani.

### JINSI YA KUADHIBU

SARUFI (S) = Adhibu makosa 6x ½ = al 3
HIJAI (H) = Adhibu makosa 6x ½ = al 3
ZIADA (Z) = Kwa **maneno 10 ya kwanza** yaliyozidi yale yaliyoagizwa katika maswali yote,

adhibu alama 1

= kwa **kila makosa mengine 5 zaidi**, adhibu alama ½ kila yatokeapo hata kama ni mangapi.

### TANBIHI

JINSI YA KUSAHIHISHA - UFAHAMU, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII

1. Weka alama alizopata mtahiniwa baada ya jibu lake. Kama amekosea, mpe sufuri "0". Usiweke alama za kusahihisha (**x** au ✓) kuonyesha kukosa au kupata.
2. Baaba ya kutuza alama, soma jibu lake tena ukitafuta makosa ya sarufi na hijai. Pigia mstari kila kosa linapotokea.
3. Kwa kila kosa la sarufi katika kila jibu, andika alama ya "**S**" baada ya alama ulizomtuza

na "**h**" kwa kila kosa la hijai. Jumla ya makosa ya hijai katika maswali yote (ufahamu,

Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu jamii ni 6x ½ (al 3 kwa kila swali)

4. Kila kosa huadhibiwa nusu alama. Kwa makosa ya sarufi utaadhibu hadi nusu ya alama ulizomtuza.

Kama hajapata alama katika swali husika au kufanya makosa zaidi ya nusu ya alama alizopata, utayapigia mstari iakini hutaonyesha baada ya jibu wala kuyaadhibu.

5. Utaadhibu makosa yote ya hijai hata kama hajapata alama yoyote katika swali hilo.

6. Ikiwa mtahiniwa amarudia kosa lile lile km. matumizi ya herufi ndogo badala ya kubwa, utaadhibu mara mbili za kwanza katika maneno mawili tofauti. Yakitokea tena utaonyesha tu kwa kupigia mstari iakini hutadhibu.

7. Katika Ufahamu, Matumizi ya lugha na Isimu jamii, makosa ya sarufi huadhibiwa hadi nusu alama alizopata katika kila kisehemu, a), b), c) nk ya alama ALIZOPATA si zile ZILIZOTENGEWA kisehemu cha swali hilo.

8. Katika ufupisho, hijai na sarufi huadhibiwa jumla ya makosa 6X ½ (al. 3) kila moja – anaweza kupoteza jumla ya alama 3 za sarufi na 3 za hijai

## BAADHI YA MAKOSA YA SARUFI.

**(Hili ni kosa lolote linalopotosha sarufi)**

1. Upatanisho mbaya wa kisarufi- **km mbuzi zao (mbuzi wao)**
2. Uakifishaji usiofaa- alama za uakifishaji, matumizi ya herufi kubwa na ndogo, nk
3. Miundo mibaya ya sentensi
4. Mnyambuliko usiofaa wa vitenzi
5. Kuacha neno katika sentensi
6. kuongeza neno katika sentensi nk

## BAADHI YA MAKOSA YA HIJAI.

**(Hili ni kosa lolote linaloathiri matamshi)**

1. Kutenganisha maneno km. Aliye kuwa.
2. Kuunganisha maneno km. Kwasababu, kwanini nk.
3. Kukata silabi mwishoni mwa sentensi km.......................................................... "Nitak - uja," (badala ya.......................................................................... "Nitaku - ja")
4. Kutoweka kistari anapotenga neno
5. Kubadilisha herufi km. **L/r, p/b , s/z/ch/sh t/d** nk
6. Kuacha herufi katika neno **km. Aliekuja (aliyekuwa)**
7. Kuongeza herufi katika neno **km. Piya (pia) ndirisha(dirisha)**
8. Kutokamilisha neno km. **Bab** na **mam**
9. Kuweka kistari pahali pasipofaa **km ali-kuwa.**
10. Kuacha ritifaa katika sauti za ving'ong'o **km. ngombe, ngangana**

Matumizi ya lugha

- Majibu

(a) (i) /b/ Ghuna

/p/ Sighuna

(ii) /dh/ Menoni 1X1

/ch/ Kaakaa gumu 1X1

(b) (i) Usafi wake ulitufurahisha 1X1

(ii) Kiatu safi, mioto safi n.k. 1X1

(c) Vijisahani hivyo vimechafuliwa na mikono yao. 1X1

**Ritifaa/Kibainishi** 1X1

(d) (i) Kuonyesha kuwa sauti / herufi Fulani imeachwa kwa mfano, 1X2

Siniudhi, N'chamchukua n.k.

- Kuonyesha sauti za ving'ong'o. Mf. Ng'ata, ng'ombe n.k
- Kuonyesha silabi iliyotiliwa mkazo mfano

Ba'rabara

Bara'bara

- Kuonyesha matumizi ya shadda

Baba'raba

a'mua

Si'mama

(ii) Parandesi /( )/ **(Zozote 2)** 1X2

- Kufungia maelezo ambao ni ufafanuzi wa jambo.

Aka (hutumika kwa kistaajabu)

- Kufungia neno ambalo ni kisawe m.f

Mishororo (mistari)

- Kufungia maelezo ya ziada pembeni.

Mf.

Mvua ikinyesha vaa viatu (kama kweli unavihitaji).

- Hutumika kifungia herufi na nambari katika kuorodhesha. M.f

(a) 2

(b) (f)

n.k.

(e) Mwanagenzi **(Zozote 2)**

Ngeu

(f) a - nafsi 2X1

Li - wakati

m - Mtendewa

gomb - shina

ez - kiendelezi

a - Kiishio

(g) Mwanafunzi aliyesoma (Kishazi tegemezi) **(6X ½ = 3)**

Amefuzu mtihani (Kishazi huru)

(h) Yule mwanabiashara (Kirai kiwakilishi) 2X1

Amepata hasara kubwa (Kirai kitenzi)

Hasara kubwa (kirai nomino)

(i) Baba alimlaani mwanawe muasi (Zozote 2) (2X1) = 2

(j) Susan hakufanya kazi kwa bidii wala kufanikiwa maishani.

Susan hakufanya kazi kwa bidii na hakufanikiwa maishani.

(k) Uchanganuzi




Kila hoja ni ½ alama 16X ¼ =4

(l) Mfano wa sentensi ya nomino ya dhahania mf.

- Ushetani wake unaudhi
- Ukora, werevu, utundu. N.k.

(m) Baba alimwamuru aende hapo /pale/ alipokuwa

(ii) Msichana alimwambia mpenzi wake waende kwao siku hiyo jioni. 1X2

(n) Baba aliyemzaa amefika 1X2

Baba anaambiwa kuwa mzazi Fulani amefika.

- Babu amefika.

(o) Ndiye - kitenzi kishirikishi kipungufu.

Aliyekuwa - kitenzi kishirikishi kikamilifu

Akisomesha - Kitenzi kikuu

(p) Karatasi - I – ZI 3X1

Nyasi - ZI (U – ZI)

(q) Kimeliwa

(r) Nne 2X1

(ii) Parandesi 1X1

- Hutumiwa kufungia maneno au ufafanuzi wa kifungu.

Mf. Aka (hutumika kwa kustaajabu).

(d) Mwanagenzi

4. ISIMU JAMII

(a) Sajili ya sheria 1 x 2 = 2

(b) X - Kiongozi wa mashtaka

Y - Mshtakiwa 2 x 1 = 2

(c) (i) Lugha ya unyenyekevu na heshima – ikiwezekana

(ii) Msamiati maalum – Kukata rufani

(iii) Lugha dadisi – Ulisema unataka kukata rufani

(iv) Kubadili msimbo – umepata presidential amnesty

(v) Kuzingatia sarufi – Nitaenda kanisani Ijumaa kuabudu na kumshukuru Mungu.

3 x 2 = 6

Jumla 10